MAELEZO KUHUSU TARATIBU ZA KUINGIZA NA KUTOA MIZIGO YA WATANZANIA WANAOISHI UGHAIBUNI

1.0 Utangulizi

Diaspora wa Kitanzania ni mtu yeyote ambaye ni raia au asiye raia wa Tanzania lakini anauasili (origin) wa Kitanzania ambaye kwa sasa anaishi na kufanya kazi au biashara kwenye nchi za Ughaibuni (foreign countries).

Diaspora wa Kitanzania ambao wanaamua kurejea nyumbani baada ya kukaa nje ya nchi kwa kipindi kinachozidi miezi kumi na mbili hawatozwi Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), Ushuru wa Forodha wala Ushuru wa Bidhaa pale wanapowasili nchini kwa mara ya kwanza tangu waondoke nchini. Msamaha huu unawahusu watu wazima wote wenye umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea. Bidhaa au mali zitakazohusika zinatakiwa kuwa ni zile ambazo Diaspora alikuwa anazimiliki wakati akiwa nje ya nchi. Bidhaa hizi ni mavazi, vyombo vya ndani, pamoja na gari moja lenye uwezo wa kupakia abiria chini ya 13 na awe amelimiliki kwa muda usiopungua miezi kumi na mbili.

Diaspora wa Kitanzania wenye nia ya kusaidia ndugu zao, makundi ya Watanzania au kuwekeza nchini ni muhimu kujua haki zao za kikodi na wajibu wao kabla hawajatuma bidhaa/mali au misaada kwa ndugu zao waishio nchini.

2.0 Misaada kwa Asasi za kijamii (Charitable Organizations)

Diaspora wa kitanzania wanaweza kutoa misaada kwa Asasi za kidini (Religious Organisations) na Asasi za kijamii (NGOs) zilizoandikishwa kisheria na misaada hiyo itapata msamaha wa kodi ya Ushuru wa Forodha (Import Duty), Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) na Ushuru wa Bidhaa (Excise Duty).

Sheria ya Ongezeko la Thamani (VAT Act, 2014) kupitia Jedwali la misamaha la Sehemu ya II (Part II) linatoa misamaha ya kodi kwa chakula, nguo, na viatu vilivyoingizwa nchini na NGOs kwa ajili ya misaada kwa yatima au shule za watu wenye mahitaji maalum ndani ya Tanzania Bara. Vile vile, msamaha umetolewa katika uingizaji

wa bidhaa kupitia NGOs ambazo zitatumika nyakati za dharura au majanga ya kitaifa. Sehemu ya 6 ya Jedwali la misamaha la Sehemu ya II inasema "*An import of food, clothing and shoes donated to non-profit organization for free distribution to orphanage or schools for children with special needs in Mainland Tanzania*", wakati sehemu ya 7 ya Jedwali hilo inasema "*Import of goods by non-profit organization for the provision of emergency and disaster relief, and where such goods are capital goods, the goods shall be handled to the National Disaster Committee upon overtion, completion or diminishing of the disaster.*"

Vile vile, Serikali kupitia Tangazo la Serikali Na. 205 na 206 (GN 205 and GN 206) ya tarehe 30 Juni, 2016 imefanyia mabadiliko kwenye Sheria za Ushuru wa Forodha (The Customs Management and Tariff Act, (CAP 403)) na Ushuru wa Bidhaa (The Excise Management and Tariff Act, (CAP 147)) kwa kuanza kutoa misamaha kwa Taasisi za Kidini pamoja na NGOs zinazoingiza bidhaa nchini kwa madhumuni ya kuendeleza dini, dharura, kusaidia majanga, miradi ya kielimu, afya, usambazaji wa maji, ujenzi wa miundo mbinu n.k. Misamaha hii hutolewa pale tu Taasisi hizi zinapotimiza masharti maalum kama ilivyoainishwa katika Sheria hizi.

Sheria ya Kodi ya Mapato, The Income Tax Act CAP 332 (2004) kupitia kifungu 64 (1) – (8) imeelezea utaratibu wa kuzitoza kodi Taasisi za Kidini na zisizo za Kiserikali zinazofanya shughuli zake hapa nchini. Kifungu cha 64 (1) kinatafsiri "*A charitable organisation or religious organisation shall be treated as conducting a business with respect to its functions referred to in subsection (8) as the "charitable business.*"

Maombi ya Msamaha yaelekezwe kwa Kamishna wa Forodha na Ushuru wa Bidhaa na yanatakiwa kuwasilishwa na Taasisi inayonufaika na msaada. Hivyo basi Diaspora wa Kitanzania anayetoa msaada atambue kuwa nyaraka zote za mzigo husika zinatakiwa zisome jina la asasi inayonufaika na msaada huo.

3.0 Mchakato wa Utoaji wa Msamaha wa Kodi

Asasi za kijamii, Asasi za kidini au Asasi zisizo za Kiserikali (NGOs) zinazosamehewa kodi ni zile ambazo zinafanya kazi ya utoaji huduma zisizo za kibiashara kwa jamii zilizosajiliwa kisheria kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani. Ni wajibu wa mpokeaji wa misaada kutoka kwa Diaspora kufuata utaratibu wa kiforodha wa kutoa mizigo bandarini kupitia mawakala wa forodha waliosajiliwa na TRA. Mpokeaji wa mizigo atapaswa awasilishe nyaraka zote za mzigo huo na kumkabidhi wakala wa forodha. Wakala wa forodha ndiye mwenye wajibu wa kutengeneza kadhia za forodha kwa ajili ya kuomba msamaha wa kodi husika.

Ili msamaha uweze kutolewa nyaraka zifuatazo zinatakiwa kuwasilishwa kwa Kamishna Mkuu na mpokeaji wa msamaha:-

i. Barua ya kuanzishwa kwa Asasi husika kutoka kwa Mkuu wa Wilaya na Afisa Mtendaji wa Kata kuthibitisha uwepo wa mradi, msiba wa asili, hatari au maafa;
ii. Barua iliyoandikwa na Mkuu wa Shirika la Kidini au Asasi zisizo za Kiserikali au mtu anayesimama kwa niaba yake kuwa ni mmiliki wa bidhaa au huduma zinazoingizwa au kununuliwa kwa mujibu wa mpango wa ununuzi wa Shirika husika;
iii. Taarifa ya kina ya uhasibu kwa matumizi ya bidhaa zilizosamehewa kodi kwa kipindi kilichopita itumwe kwa Kamishna Mkuu mwezi mmoja baada ya kumalizika kwa kila mwaka wa Fedha.

Msaada uliotolewa utaacha kuwa halali na Kodi ya Ushuru kulipwa kama vile msamaha haujatolewa, ikiwa bidhaa hizo zitahamishwa, zimeuzwa kwa namna yoyote kwa mtu mwingine asiyehusika.

4.0 Bidhaa Zinazokidhi Vigezo vya Kupata Msamaha

Kama nilivyokwisha elezea hapo juu, misamaha kwa Asasi za kidini pamoja na NGOs hutolewa kwa bidhaa zinazoingizwa Nchini kwa madhumuni ya kuendeleza dini,

dharura, kusaidia majanga, miradi ya kielimu, afya, usambazaji wa maji, ujenzi wa miundombinu n.k. Misaada hii hutolewa pale tu Taasisi hizi zinapotimiza masharti maalum kama ilivyoainishwa Katika Sheria husika.

Kwa Diaspora Wakitanzania wenye kumiliki au kudhamini NGO's, hawatapata msamaha wa Kodi ya VAT kwa uingizaji wa bidhaa za ulaji (consumables) kama vyakula, vinywaji, vipuri, magari, pikipiki na vifaa vya ujenzi.
Zifuatazo ni nyaraka muhimu zitakazotumika kutoa msamaha wa kodi kwa uingizaji wa bidhaa zilizosamehewa kodi.

i. Nyaraka za usafirishaji (Bill of lading or Airway Bill)
ii. Risiti za bidhaa zilizopo (Invoice or Packing list of the goods)
iii. Cheti cha kupewa msaada (Donation Certificate)
iv. Cheti cha usajili wa Shirika kutoka kwa msajili wa Asasi (certificate of registration of the organization from the registrar of societies)
v. Barua ya uhakiki wa Shirika kutoka kwa Mkuu wa Wilaya (letter from the District Commisioner to confirm the existence of the charitable organization or NGO on the receipient's area)